# Usimulizi katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia

*Samson Ontiri Ongarora*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Kithaka wa Mberia ni mtunzi wa mashairi huru. Ametunga diwani kadhaa za mashairi huru yenye maudhui anuwai na masuala ibuka. Katika kuangazia maudhui mbalimbali katika ushairi wake, ametumia mbinu ya usimulizi katika baadhi ya mashairi katika diwani zake. Usimulizi unatumika sana katika utambaji wa hadithi katika fasihi simulizi na katika tanzu za riwaya na hadithi fupi katika fasihi andishi. Ni nadra sana usimulizi kutumika katika ushairi. Ingawa tenzi ndizo zinahusishwa na usimulizi kama vile katika Utenzi wa Fumo Liyongo (1913), inawezekana mashairi mafupi yakawa na sifa ya usimulizi kama tunavyoona katika mashairi ya Kithaka wa Mberia. Katika makala haya, tunajadili aina za usimulizi katika baadhi ya mashairi yake katika diwani zake nne ambazo ni: Mchezo wa Karata (1997), Bara Jingine (2001), Redio na Mwezi (2005), na Rangi ya Anga (2014). Matumizi haya ya mtindo wa usimulizi ndiyo yanayoupa ushairi wake ubunifu mpya, usasa na upekee fulani.**

**Maneno Muhimu:** Usimulizi, Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza, Usimulizi wa Nafsi ya Pili, Usimulizi Mwakote.

## Utangulizi

Usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Wamitila (2008) anasema kuwa mtazamo unaochukuliwa katika usimulizi wa kisa chochote au matini yoyote huwa muhimu kwa sababu ni mbinu ya kimtindo ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa uelewekaji wa matini yenyewe. Aidha, mkabala anaochukua msimulizi unaweza kuonyesha msimamo wake kuhusu hali fulani au anajitambulisha na nani. Kwa sababu hiyo, tunaamini kuwa mikabala anayoichukua mshairi huyu inaonyesha misimamo yake kuhusu hali fulani na wahusika anaojitambulisha nao. Katika makala haya, tunachanganua namna Kithaka wa Mberia ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya pili, nafsi ya tatu na usimulizi mwakote katika kuwasilisha maudhui mbalimbali katika utunzi wake.

## Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza

Katika aina hii ya usimulizi, mshairi anatumia kiwakilishi cha nafsi ya kwanza "mimi" mbali na kutumia mofu "na" na "ni" kurejelea njeo na nafsi mtawalia ili kupunguza umbali kati ya kinachosimuliwa na msomaji. Mshairi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza anapoangazia maudhui kuhusu mazingira. Kwa mfano, katika shairi "Mimi, Mto Nairobi" (uk. 63) katika diwani ya *Bara Jingine,* ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza (mimi) kueleza namna mto Nairobi unavyochafuliwa kwa taka anuwai na wakaazi wa Nairobi. Mshairi anasimulia:

1. Wakaazi wa jiji
Wa**nani**kaba koo
Wa**nani**ziba pumzi
Wa**nani**nyonga…(uk. 63)

Katika shairi hili, mwandishi anazungumzia juu ya uharibifu wa mazingira. Uharibifu wa mazingira ni wa aina nyingi. Kuna uharibifu wa ardhi, hewa, maji, miti na kadhalika. Mshairi amelenga juu ya uchafuzi wa mto Nairobi. Mtunzi anasema kwamba wakaazi wa Nairobi wana mazoea ya kuchafua mto huu kwa kutupa takataka za kila nui kama vile nguo kuukuu, karatasi, majitaka kutoka viwandani, mipira ya plastiki, matairi ya magari miongoni mwa takataka zingine. Maji ya mto Nairobi yakishachafuliwa hayawezi kutumiwa tena. Viumbe wa majini hasa samaki huuawa na sumu iliyochanganyika na maji.

Mshairi, kupitia nafsi ya kwanza "mimi" anajiweka katika hali ya mto huu ili kumsaidia msomaji kuelewa ni vipi mto huu umechafuliwa na pengine kuchukua hatua madhubuti za kuunusuru dhidi ya uchafuzi zaidi. Aidha, kupitia usimulizi huu wa nafsi ya kwanza, mshairi anaonyesha msimamo aliouchukua kuhusu umuhimu wa kutunza au kuhifadhi mazingira.

Aidha, kuna usimulizi wa nafsi ya kwanza mshairi anaposifu uzuri wa mti aina ya mjakaranda katika shairi "Mjakaranda" (uk. 75) katika diwani hii ya *Bara Jingine*. Anatumia mbinu ya usimulizi kupitia mbinu rejeshi. Anatumia mbinu rejeshi (nakumbuka) na mofu "li" kurejelea wakati uliopita. Anasimulia:

2. **Nakumbuka** siku ambayo
Macho yetu ya**li**kutana
Nyoyo zetu zi**ka**pendana
Mapenzi ya**ka**umana
Ni**li**kuwa Parkview ghorofani…(uk. 75)

Katika shairi hili, mtunzi anaeleza jinsi mti huu aina ya mjakaranda ulivyopendeza machoni mwake mbali na kuyapamba mandhari kwa maua yake ya rangi ya urujuani katika bustani ya Jevanjee iliyoko jijini Nairobi. Neno "nakumbuka" linaashiria sifa ya usimulizi wa matukio yaliyopita. Fauka ya hayo, mofu "li" na "ka" zinadhihirisha mfuatano wa vitendo. Kupitia usimulizi huu, tunapata msimamo wa mshairi juu ya mazingira safi na pendezi yanayotokana na miti ya mijakaranda katika bustani hilo.

Isitoshe, mwandishi anaposimulia safari yake na wenzake kwenda Malindi kujivinjari, anasimulia kwa kutumia mofu "tu" ya nafsi wingi na mofu "li" kuonyesha wakati uliopita. Anasimulia katika shairi "Kambi Malindi" katika diwani hii ya *Bara Jingine* kwa nia ya kuonyesha jinsi hali ilivyokuwa mbali na kudhihirisha mpito wa wakati. Anasimulia:

3. **Tuli**fika alasiri
Jua lilikuwa na upole…
Bahari **ilitu**karibisha…
Ufukwe **ulitu**pokea…(uk. 79)

Katika shairi hili "Kambi Malindi", mshairi anasimulia hatua kwa hatua safari yao kwenda Malindi. Usimulizi huu unajitokeza sawa na mtu anayeeleza msikilizaji fulani kiasi cha kutekwa akili na maelezo hayo. Anapoeleza kuwa "tulifika alasiri, jua lilikuwa na upole…", msomaji anaanza kupata taswira kuwa miale ya jua haikuwa inachoma sana wakati huo wa alasiri. Aidha, anatumia tashihisi pale anaposema kuwa bahari iliwakaribisha na ufukwe kuwapokea. Matumizi ya tashihisi hizi yanafanya usimulizi huu kutoa taswira ya mandhari tulivu ya ufuo wa bahari yanayovutia watalii na wanaopenda kuogelea.

**Usimulizi wa Nafsi ya Pili**

Katika usimulizi wa nafsi ya pili, mshairi anatumia mofu "u" au "wewe" kurejelea mhusika mkuu kuhusu yaliyomtendekea, kuelezea kitu au hali fulani. Usimulizi wa nafsi ya pili una athari kwa hadhira kwa sababu unanuia kumleta karibu msomaji au hadhira kwa kuihusisha na matukio yanayosimuliwa. Kwa mfano, katika shairi "Pamela" (uk. 28) katika diwani ya *Bara Jingine*, mshairi anatumia mofu "u" kumrejelea Pamela ambaye alinajisiwa na kundi la wavulana walevi alipokuwa akitoka shuleni jioni moja. Anasimulia:

4. Taratibu
Kama mto ambao
Unakaribia bahari
Pamela **ali**fuata mapindo ya njia…
**Uli**pokanyaga mtego
Wa**liku**shambulia…
Nawe, Pamela
**Uli**bakia gizani… (kur. 29-30)

Katika shairi hili, mtunzi anaeleza kwa uchungu namna msichana wa shule alibakwa na kundi la wavulana walevi. Visa vya ubakaji vinaripotiwa kwenye vyombo vya habari kila kuchao. Visa hivyo vinatendewa wakongwe, wanawake wa umri wa makamo, wasichana na watoto wachanga. Msichana kwa jina Pamela alitendewa kitendo hicho cha ukatili alipokuwa anarejea nyumbani akiwa peke yake baada ya masomo ya mchana kutwa. Hakuwa na habari kuwa kulikuwa na wavulana waliokuwa wanamwotea njiani kwa nia ya kumdhulumu kimapenzi.

Usimulizi wa mshairi unatupatia taswira namna Pamela alifuata njia taratibu akielekea nyumbani sawa na mto unaokaribia baharini. Ghafla, alishikwa kwa nguvu na wavulana walevi. Walimrarulia sare yake ya shule, mkoba kisha wakatapanya vitabu vyake. Walimwangusha chini na kumdhulumu kwa zamu. Hatimaye, waliondoka na kumwacha hapo akiwa hoi huku wakishangilia kuwa alikuwa bikira. Kitendo hicho kiliathiri masomo yake kwa sababu aliacha kusoma na akawa mwendawazimu aliyezurura sokoni akiokota vitakataka, kutokwa na matusi mbali na kutembea uchi. Msomaji anapata taswira ya huzuni na huruma kwa msichana aliyetia bidii masomoni lakini ghafla ndoto zake zikazimwa na vijana wahuni.

Kupitia usimulizi huu, mshairi anaonyesha wazi madhara ya ubakaji kwa wasichana wa shule ambao wana matumaini makubwa juu ya maisha mema katika nyakati zao za usoni. Wanapodhulumiwa kimapenzi, maisha yao yanaingia giza kwa kuachiwa kovu lisilopona. Kwa mujibu wa mtunzi, ubakaji ni uovu unaostahili kupingwa vikali na washukiwa kuchukuliwa hatua kali kisheria.

Hali kadhalika, upo usimulizi wa nafsi ya pili katika shairi "Mgeni Katili" (uk. 4) katika diwani ya *Redio na Mwezi.* Mtunzi anatumia nafsi ya pili kusimulia juu ya ugonjwa mgeni ambao ni ukimwi. Anasema "**Wewe**, katili, jambazi la kutisha …"(uk.4). Katika shairi hili, mwandishi ametumia mofu "wewe" kueleza madhara mbalimbali ya ugonjwa wa ukimwi kwa wanajamii. Mshairi anasema kuwa ugongwa wa ukimwi unawaua wanawake kwa wanaume. Anaonyesha taswira ya kuogofya jinsi ugonjwa huo unawakamua kila tone la uhai na kuwatupa kaburini wakavu kama kuni. Picha ya namna hii inashtua. Mtunzi anasisitiza kuwa ugonjwa wa ukimwi haubagui wala kujali hadhi ya mtu. Unawaua wasomi, wazazi, viongozi wa nchi, mawaziri, wabunge na maofisa wa polisi wa ngazi za juu na chini. Madhara ya vifo vya watu hao wote ni kwamba wanaacha msururu wa watoto mayatima ambao wanateseka kwa ukosefu wa malezi mazuri, mahitaji yao ya kimsingi na elimu nzuri.

Aidha, katika shairi "Rafiki Katili" (uk.57) katika diwani hili ya *Redio na Mwezi* mshairi ametumia nafsi ya pili kusimulia juu ya madhara ya pombe kwa walevi. Mtunzi anasema kuwa pombe ni rafiki ya mlevi ambaye humpa mlevi ujasiri bandia, udanganyifu, uropokaji ovyo wa maneno mbali na kuzua fujo miongoni mwa mambo mengine. Mwandishi anatumia mofu "wewe" na "u" kusimulia juu ya pombe. Kupitia kwa masimulizi haya ya nafsi ya pili, tunaona matokeo ya pombe kwa mlevi na madhara anayofanya kwa watu wengine. Anaeleza:

5. Tembo, **wewe** ni sungura mjanja
Shujaa wa uzandiki na unafiki
Bingwa wa uwongo na udanganyifu
**U**nachezea akili na kuifanya butu
**U**nawarairai, unawadanganya
**U**nawatawala watu kwa mamlaka imara
**U**nawafanya kuropokwa na maneno….(kur. 57-58)

Miongoni mwa madhara ya pombe kwa wanywaji wa kileo hicho ni kuwa wanatembea kwa kuyumbayumba, wanaropokwa na matusi mabaya, wanaenda wakimwaga udenda na wengine kulala ndani ya mitaro. Fauka ya hayo, tembo linachangia watu kufarakana na kupigana ngumi kiasi cha kung'oana meno ilhali wengine huumizana uso na mashavu kupitia vigae vya chupa za pombe. Hali kadhalika, walevi wengine wanaua jamaa na marafiki kwa kuwakata kwa mapanga na visu vyenye makali. Madereva walevi wanashindwa kuwa makini barabarani kwa sababu hawaoni wala kuzingatia sheria za barabarani. Wanaaendesha magari kwa kasi, jambo ambalo linasababisha ajali na vifo kwao pamoja na abiria.

Mtunzi anaendelea kusimulia katika shairi hili kwamba pombe inachangia watu kuambukizana ugonjwa wa ukimwi kwa vile walevi hawana uwezo wa kudhibiti hisia zao za kimwili. Wengi wao wakiwa walevi hawaoni wanachofanya katika vilabu vya pombe kwa sababu ya raha na starehe nyingi. Isitoshe, anasema kuwa tembo husababisha miereka nyumbani, ugomvi na kufanya nyumba kuwa ulingo wa vita. Inakuwa rahisi kwa mwanandoa kumpiga risasi, kumchoma kisu au kumkata mwenzake kwa panga. Badala ya ndoa, kunabaki jivu.

Kwingineko, katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya nne katika diwani ya *Rangi ya Anga,* mtunzi anatumia usimulizi wa nafsi ya pili kueleza mateso anayopitia mwanamke anayejifungua watoto wa kike tu. Anatumia mofu “wewe” na “u” kwa kurudiarudia kumrejelea mwanamke huyo. Anasimulia:

6. **Wewe** mwenye sauti nyororo
Na maungo mviringo na laini
**Wewe u**sonywaye maishani
Na wenye taasubi ya jinsia,
**Wewe u**bezwaye **u**naposema
Na kutwezwa **u**napotenda,
**Wewe u**dharauliwaye sokoni
Na kudhalilishwa nyumbani,
**Wewe u**kemewaye mezani…(uk. 6)

Katika dondoo hili, mshairi anasimulia mateso ya mwanamke ambaye hawezi kujifungua mtoto wa kiume katika ndoa yake. Mwanamke anayejikuta katika hali hiyo anasonywa, anabezwa, anatwezwa, anadharauliwa, anadhalilishwa na anakemewa kwa kosa ambalo si lake. Mambo hayo yote yanamfanya mwanamke kukosa amani katika ndoa yake. Anakuwa na mzongo wa mawazo ni siku gani atabarikiwa kupata mtoto wa kiume ili aondokewe na udhia wa jamaa, marafiki na watu wengine wenye umbeya katika jamii kuhusu hali yake.

Wenye taasubi za kiume wanaamini kuwa ndoa huwa imekamilika ikiwa mwanamke amepata mtoto wa kiume. Hata baadhi ya wanawake wanamini hivyo na ndio sababu utaona mama akiendelea kuzaa watoto ili kujaribu bahati yake ya kupata mtoto wa kiume. Matokeo yake ni kwamba wanandoa wanaishia kuwa na watoto wengi ambao labda ni shida kuwalea vizuri au kuwasomesha. Ujumbe wa mshairi katika shairi hili ni kwamba mtoto ni mtoto, awe wa kiume au wa kike. Imani kwamba mtoto wa kiume ni wa thamani zaidi kushinda wa kike ni potofu na imepitwa na wakati. Mwanamke hafai kuonewa na kudhalilishwa kwa jambo asilokuwa na uamuzi kwalo.

**Usimulizi wa Nafsi ya Tatu**

Katika usimulizi wa nafsi ya tatu, mtunzi anatumia mofu “a” na “li” kuelezea matukio mbalimbali. Katika shairi “Rangi ya Anga” (uk. 1) sehemu ya kumi katika diwani ya *Rangi ya Anga,* mshairi anaeleza vile mvulana na msichana walianza urafiki wa kimapenzi walipokuwa shuleni. Kwa bahati mbaya msichana alikuwa mjamzito kisha akafukuzwa shuleni ilhali mvulana aliyemringa aliendelea na masomo yake, akahitimu, akapata kazi nzuri na kuishi maisha ya kifahari. Lakini msichana aliyefukuzwa shuleni aliishia kuwa maskini na kahaba mjini ili amkimu mtoto wake. Mshairi anasimulia hivi:

7. **Wali**kuwa wachanga
Katika kivuli cha shule
Hisia za ujana **zili**povutana…
Mmoja wa wawili washiriki
**Ali**endelea na mwendo shuleni
**Aka**kusanya vyeti vya maana
Na kupata jina adimu nchini,
Leo, asubuhi, **a**nakula mayai
Na asali na siagi ya thamani,

**Ana**valia mavazi ya kuteua… (uk. 13)

Katika shairi hili, mtunzi anasimulia juu ya matokeo ya mapenzi haramu kati ya mvulana na msichana ambao wanasoma shuleni. Anadhihirisha kuwa katika mapenzi ya aina hiyo, msichana ndiye anapata hasara kubwa. Msichana akihimili, atalazimika kuacha shule ili kulea mimba na mtoto wake. Lakini mvulana anayehusika na kitendo cha kumringa msichana, ataendelea kusoma hadi chuo kikuu. Hatimaye, atapata kazi nzuri na kuishi maisha mazuri ilhali msichana huyo atadidimia katika upweke, lindi la umaskini na labda kuwa windo jepesi kwa wanaume kusudi apate kumkimu mtoto wake.

Ujumbe wa mshairi katika shairi hili ni kwamba wazazi na wasimamizi wa shule wasimnyanyase mtoto wa kike pale anapokuwa mjamzito kwa kumnyima nafasi ya kuendelea kusoma ili naye atimize ndoto zake maishani. Aidha, anawaonya wasichana wasiingie katika mtego na ujanja wa wavulana wa kushiriki mapenzi haramu bali watazame maisha yao ya mbeleni.

Aidha, katika sehemu ya kumi na mbili ya shairi "Rangi ya Anga", mshairi anatumia nafsi ya tatu kueleza vile msichana mmoja alichukuliwa na wakala kutoka kijijini kwenda mjini kufanya kazi ya uyaya. Akiwa huko, mwajiri wake wa kiume alifanya mapenzi na huyo msichana kisha akawa mjamzito. Baada ya mke kugundua siri ya ujauzito wake, alimfurusha kutoka nyumbani mwake. Baadaye, msichana huyo alijifungua mtoto wakaanza safari ngumu ya maisha ya umaskini. Mwandishi anasimulia:

8. Kwa ahadi tamutamu kama halua
Wakala **ali**mrairai mama-mzazi
**Aka**mnyakua binti kutoka shamba
**Aka**mbwaga kwenye vimetemete jijini
Kutunza watoto wa watu mtaani
Kupigana na miereka na kazi za jikoni
Na kuipa nyumba sifa kwa unadhifu. (uk. 17)

Kimsingi, dondoo hili linasimulia safari ya msichana mmoja kutoka kijijini hadi mjini kwenda kufanya kazi ya uyaya. Alipofika huko kwa mwajiri wake, alianza kufanya kazi ya kutunza watoto, kupika na kuosha vyombo jikoni mbali na kupiga deki nyumba. Lakini mwajiri wake wa kiume alianza kumtaka urafiki wa kimapenzi kisiri bila mke wake kujua. Alimshawishi kwa kumpatia zawadi ndogondogo kama pesa za ziada za kujinunulia mahitaji yake, hanchifu, chokoleti, mafuta na mavazi ya ndani. Msichana aliridhia matakwa yake kisha wakashiriki mapenzi naye. Baadaye, alipata ujauzito ambao mwajiri wake wa kike aligundua na kumfukuza. Kupitia usimulizi huu, mshairi anamulika mateso na majaribu wanayopitia mijini mikononi mwa waajiri wao wale wasichana wanaofanya kazi ya uyaya.

**Usimulizi Mwakote**

Usimulizi mwakote ni mkabala wa usimulizi ambapo mwandishi anajua tabia za wahusika na hata fikira zao. Mohamed (1995) anasema kuwa usimulizi mwakote ni sauti inayojua yote, ya ndani na ya nje; sauti inayoangazia mahali, matukio, hisia, maumbile na tabia za wahusika na saikolojia zao. Msimulizi huingia apendavyo na atakavyo kwa uhuru na kisha kutoa habari atakavyo. Kwa hivyo, katika usimulizi mwakote, msimulizi anajua na anaeleza yote.

Katika shairi "Mlipuko wa Furaha" (uk. 56) katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, mshairi anasimulia jinsi simba alivyong'olewa meno na kucha ndipo wanyama wengine wakapata uhuru mbugani. Katika shairi hili, simba anawakilisha kiongozi dhalimu, wanyama wanawakilisha wananchi na mbuga inawakilisha nchi aliyoitawala kiongozi huyo. Mwandishi anasimulia:

9. **Siku zikapita**
**Simba akinguruma**
**Na kutabasamu**
**Siku zikapita**…
**Jogoo akawika**…

Kutoka anga 'tulivu'
**Mawingu yalitanda**
**Kimya kikayeyuka**
**Mbingu zikatetemeka**
Nguvu zisizozuilika
Zikamkabili simba
Na kumng'oa meno
Na kucha
Mbuga ikalipuka
Kwa furaha
Ya uhuru (uk. 56-57)

Katika dondoo hili, mshairi ametumia usimulizi mwakote kueleza namna simba yaani kiongozi fulani alitawala kwa udikteta miaka mingi akiwa na kiburi. Utawala wake ulikuwa wa dhuluma kwa watawaliwa. Wananchi yaani wanyama walipochoshwa na utawala wake, walimkabili na kumng'oa mamlakani na kujipatia uhuru. Haya ni maudhui ya udikteta na ujenzi wa jamii mpya kupitia mapinduzi. Dhuluma za kiongozi mwovu kwa watawaliwa hazitadumu milele. Maneno **"siku zikapita simba akinguruma na kutabasamu"** na **"siku zikapita jogoo akawika"** ni usimuli unaoonyesha mpito wa wakati na mfuatano wa matukio hadi kiongozi huyo alipong'olewa mamlakani.

Usimulizi mwakote vilevile umedhihirika katika shairi "Mgunga Shambani" (uk.20) katika diwani hii ya *Mchezo wa Karata.* Katika shairi hili, mshairi anazungumzia juu ya maudhui ya ukoloni na ukoloni mamboleo kwa mtindo wa usimulizi mwakote. Maudhui haya yanaonyesha historia ya nchi ya Kenya wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Mshairi anasimulia hivi:

10.

I
**Huko zama za nyuma**
Kwenye shamba letu la mawele
**Kulistawi** gongo la mgunga
Ambalo kwa miiba myeupe
**Lilituchoma** michomo mikali
**Tuliamua** kuling'oa
Kusudi kuyeyusha dhiki…

II

**Mafungia nyama yakawadia**
**Kisha jogoo wakawika**
**Mafungia nyama yakawadia**
**Kisha jogoo wakawika**…

III
Pale **tuli**pong'oa mgunga
Pa**li**stawi mti mwingine
Michomo i**ka**tuliza machozi
Mithili zama **za nyuma** (kur. 20-21)

Mshairi anaanza kusimulia kwa maneno "**huko zama za nyuma**" ambayo ni sawa na fomyula ya "hapo zamani za kale" katika utambaji wa hadithi za fasihi simulizi. Aidha, anatumia usimulizi wa nafsi ya kwanza hali ya wingi "tu" katika maneno "**tuliamua**", "**tulitingisha**", "**tuliusikia mshindo**" na "**pale tulipong'oa mgunga**" kuonyesha juhudi za wananchi kumwondoa mkoloni ili wajitawale. Katika usimulizi wake, mshairi anaonyesha mateso Wakenya walipata wakati wa ukoloni mkongwe. Baada ya kumwondoa mkoloni kwa juhudi kubwa waliingia katika utawala mpya wa Waafrika wenzao. Lakini uongozi na utawala wa viongozi hao uliishia kuwa wa dhuluma na mateso sawa na

utawala wa wakoloni wa awali. Huo ndio ujumbe wa ukoloni na ukoloni mamboleo katika usimulizi huu. Katika kusimulia pia, amerudia maneno "**tulilitingisha**", "**mafungia nyama yakawadia**" na "**kisha jogoo wakawika**". Urudiaji ni sifa moja ya utambaji wa hadithi katika fasihi simulizi (Wamitila, 2003). Urudiaji huu unasisitiza mpito wa wakati na mfuatano wa matukio wakati wa harakati za kutafuta uhuru nchini Kenya.

Kwingineko, katika diwani ya *Rangi ya Anga* kuna usimulizi mwakote katika shairi "Zimwi la Theluji" (uk. 48). Mshairi anasimulia yote kuhusu wageni waliokuja eneo la Afrika Mashariki. Wageni hao ambao ndio "zimwi la theluji" ni Waarabu, wamishenari na wakoloni. Anaeleza kuhusu ujanja na madhila ya wageni hao kwa wenyeji wakati wa ung'ang'niaji na ugavi wa bara la Afrika. Ametumia usimulizi mwakote kueleza walivyokuja Waarabu kisha wamishenari ifuatavyo:

11. Kwa kunyemelea
**Lilikuja zimwi jeupe**
Kwanza kwenye upwa
Ambapo upepo
Hupuliza manukato ya chumvi

**Kama wimbi la maji**

**Zimwi lilisambaa**
**Na kufikia maeneo mapya**…
**Lilifuata mkondo wa wakati**
**Likavuka nyika na misitu**… (kur. 49-50)

Katika dondoo hili, msanii amesimulia vile Waarabu walikuja kwenye upwa wa Afrika Mashariki na kukaa na wenyeji. Baadaye walianza kuingia sehemu za bara katika shughuli za kufanya biashara ya kutafuta pembe za ndovu na watumwa (Chiraghidin na Mnyampala, 1977).

Baada ya ujio wa Waarabu, kundi jingine lililofuata lilikuwa la wamishenari wa Kikristo. Katika sehemu ya nne, mtunzi anasimulia hivi:

12. …**Lilikuja zimwi la theluji**
**Likibeba simulizi**
Mkururo wa vituko vya ajabu…
**Lilijidai kuwa tarishi**
Wa Muumba wa yote
**Likakunjua hadithi**
Ya Baba na Mwana
Mwana wa pekee… (uk. 51)

Katika shairi hili "Zimu la Theluji", usimulizi huu unaonyesha mjo wa Waarabu, wamishenari kisha wakoloni. Mshairi anadhihirisha hila zilizotumika na makundi yote hayo kuwatesa na kuwadhulumu wenyeji. Akitumia usimulizi, anaonyesha jinsi Waarabu na wakoloni waligeuza Waafrika kuwa watumwa, wakanyakua mashamba, wakavuruga imani na tamaduni zao kwa kuwafunza dini na elimu ngeni mbali na kudhibiti uhuru wao, kuwapiga na hata kuwaua wenyeji bila sababu yoyote.

**Hitimisho**

Katika makala haya, tumechanganua suala la usimulizi katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Tumeangazia jinsi mshairi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya pili, nafsi ya tatu na usimulizi mwakote kuangazia maudhui mbalimbali. Tumebainisha kuwa ingawa usimulizi unatumiwa katika tenzi, riwaya, hadithi fupi na ngano katika fasihi simulizi; usimulizi vilevile ni mkakati mwafaka katika uelezaji wa masuala muhimu katika mashairi mafupi. Mshairi ana uhuru wa kutumia usimulizi kuangazia na kuchimuza masuala muhimu bila kuboronga mtiririko wa mawazo yake. Fauka ya hayo, usimulizi katika ushairi wake unazua mvuto na mnato wa kisanaa. Huu ndio upekee wa kimtindo unaojitokeza katika ushari wa Kithaka wa Mberia.

**Marejeleo**

Charaghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Kijumwa, M. (1964)[1913].(Mh. J. Knappert) *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Dar es Salaam. IKR.

Mohamed, S. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Wa Mberia, K. (1997). *Mchezo wa Karata.* Nairobi: Marimba Publications Limited.

Wa Mberia, K. (2001). *Bara Jingine.* Nairobi: Marimba Publications Limited.

Wa Mberia, K. (2005). *Redio na Mwezi.* Nairobi: Marimba Publications Limited.

Wa Mberia, K. (2014). *Rangi ya Anga.* Nairobi: Marimba Publications Limited.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.